TANGAZO LA SERIKALI Na. 570 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA HASAMA HILLS YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Hasama Hills ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la hifadhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Hasama Hills.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA MBULU

MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA HASAMA HILLS

*Makadirio ya eneo:* Hekta 3815.943 au Kilomita za Mraba 38.16

Unakopatikana na Misitu

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi Hasama Hills linalopatikana katika Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 3080 ya mwaka 2021 (Skeli 1:20000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na lenye mipaka ifuatavyo:

**HASAMA HILLS FOREST RESERVE**
**MBULU DISTRICT**
**AREA 3815.943Ha OR 38.16SQ. KILOMETRES**




Dodoma,
24th Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*